# JE WAJUA?

**T**embo wana uwezo wa kuishi popote pale penye chakula na maji ya kutosha. Tembo hutumia karibu asilimia 55% ya muda wao kwa kula chakula. Hii ni kwa sababu mmeng'enyo wa chakula tumboni mwao sio mzuri. Kwa kawaida, asilimia 40-50 ya chakula ndio hutumika tu.

**T**embo hula takriban asilimia 4-6% ya uzito wa mwili wao kila siku, mfano tembo dume mwenye uzito kilo 5000 hula kilo 200 hadi 300 of majani kila siku, tembo jike mwenye uzito wa kilo 2800 huitaji kilo 112 hadi 170 cha chakula.

**T**embo hunywa takriban lita 170 hadi 230 za maji kwa wakati mmoja.

**T**embo hana PEMBE ila ana MENO. Ukmwangalia tembo vizuri utaona kuwa meno yametokezea mdomoni. Tembo hutumia meno yao katika kutafutia chakula, kujihami, kuchimbia ardhi wakitafuta maji, kuchimbia magome ya miti, kunyanyulia vitu na humsaidia kulinda mkonga wake.

**T**embo hunusa, hugusa, hupumua,hunywa maji, hupiga kelele na kushika/kunyanyua vitu kutumia mkonga wake.

**M**bali na kutumia katika kusikia, na kuashiria, masikio ya tembo huwa makubwa ili kumsaidia kupooza mwili wakati wa joto kali. Masikio ya tembo huwa na mishipa mingi hivyo wakati wa jua kali huyaachia wazi au kuyapepea ili kutengeneza nafasi ya upepo wa baridi kumfikia hivyo kupunguza joto la mwili.

**T**embo huzaliwa baada ya kipindi cha ujauzito wa miezi 22 na uzito wa kawaida wa madume huwa kilo 120, kilo 20-30 zaidi kuliko majike.Tembo huwa na uwezo wa kupata mtoto wa kwanza akiwa na umri wa miaka 12 na huendelea and wanapofikia umri wa miaka 40 na zaidi. Humchukua umri wa miaka 3-5 kupata mtoto wa pili.

**T**embo pia huwa na uwezo wa kuzaa mapacha japo hutokea kwa nadra sana. Hii imeripotiwa katika hifadhi ya Amboseli na Meru nchini Kenya.

## *Fahamu ikolojia ya tembo*

Tembo huwa madereva wakubwa wa mazingira na tegemeo kwa wanyama wengine na muhimili mkubwa katika mfumo wa ikolojia. Wakati wa kiangazi, tembo hutumia meno yao kuchimba maji. Hii huwawezesha tembo kuishi katika mazingira kavu na wakati ukame, wanyama wengine hufaidi pia maji haya.

Mazingira ya savannah yangeonekana tofauti sana bila tembo.Tembo wa Afrika hula mimea na vichaka vya miti ambapo hufungua misitu na mapori kuwa mbuga wazi ambapo hutoa nafasi kwa mimea mingine kuota na njia kwa njia za wanyama wengne.Wakati wa kiangazi tembo huangusha matawi makubwa ambayo huwawezesha wanyama wadogo kupata chakula.

Popote wanapoishi, tembo huacha kinyesi kilichojaa mbegu kutokana na mimea mingi wanayoila. Mbegu hizi huchipua na kuwa nyasi, miti na hata misitu hivyo kuongeza idadi ya mimea. Kinyesi hiki pia huongeza rutuba katika udongo hivyo kuongeza afya ya mazingira ya savannah.

Kinyesi cha tembo huwa chanzo cha chakula kwa wanyama wa aina nyingine. Wanyama kama nyani, tumbili, na ndege hutafuta mbegu katika kinyesi cha tembo.Kuna wadudu hutegemea kinyesi cha tembo kama chakula.



***Mbegu zikiwa zimechipua kwenye kinyesi cha tembo***


Landscape and Conservation Mentors Organization

**P.o. BOX 285, Mpanda Katavi**

**www.lcmo.or.tz**

Barua pepe: ***conservation@lcmo.or.tz***



**Chapisho hili limefadhiliwa na Mradi wa Rufford**




# *FAHAMU KUHUSU TEMBO WA AFRIKA*



The Rufford Foundation

www.rufford.org @ruffordgrants

LCMO

Landscape and Conservation Mentors Organization



# Tembo huwa na akili sana

Jamii kubwa ya wanyama hasa mamalia huzaliwa na ubongo asilimia 90 sawa na wale wakubwa. Hii ina maana kuwa wanahitaji kujifunza machache, asilimia 10 kutoka kwa wazazi. Hii ni tofauti kubwa sana binadamu anaezaliwa na ubongo ambao ni aslimia 28% sawa na mtu mzima. Tembo ni wanyama wenye akili sana na huwa na kumbukumbu ambazo hukaa miaka mingi. Ni kumbukumbu hizo ambazo zinawasaidia wakati wa kiangazi na wakati wanahitaji kuongoza makundi yao wakati mwingine kwa maelfu ya maili hadi kwenye vyanzo vya maji au malisho ambayo wanayakumbuka tangu zamani.

Tembo ni wanyama wanaojaliana sana na wana mifumo mizuri ya kuwasiliana na kuonyesha hisia hutumia njia zao zote za fahamu za kusikia, kuona, kunusa, kuonja na kuhisi. Vile vile ni mnyama mwenye uwezo mkubwa sana wa kusikia na kuhisi mtikisiko hata mdogo sana. Panapo hatari, tembo ni mzuri sana katika kujihami hivyo ni muhimu sana kwa binadamu kuchukua tahadhari kubwa sana wanapokua katika maeneo yenye tembo. Ni vyema kuondokana na dhana potovu ya kuwa tembo ni mnyama mkubwa na hana uwezo wa kukimbia, kukata kona za ghafla na pia kuona kuwa tembo ana macho madogo na hivyo hawezi kuona mbali. Watu wengi wamejeruhiwa vibaya na baadhi kuuawa na tembo wakitaka kupiga picha huku wakiamini tembo hawezi kuwadhuru kwa haraka.



# MNYAMA TEMBO

## Tembo wa Afrika

Kuna aina mbili za tembo ulimwenguni, tembo wa Afrika (*Loxodonta africana*) na tembo wa Asia (*Elephas maximus*) (**A**). Kwa Afrika, kuna spishi mbili: tembo wa savanna, *Loxodonta africana africana* (**B**) na tembo wa msituni, *Loxodonta africana cyclotis* (**C**). Tembo savanna ni mkubwa zaidi kuliko tembo wa msituni. Tanzania, ina Tembo wa Savanna pekee. Tembo wa msituni hupatikana Afrika ya Kati na magharibi. Tembo pia ndiye mnyama mkubwa kuliko wote waishio nchi kavu.

Uzito wake unakadiriwa kuwa kilo 6600 (tani 6.6).Tembo mkubwa katika historia alirekodiwa nchini Angola na uzito wa kilo 11,000 (tani 11), urefu wa bega ulikua mita 3.96. Alikua mita moja zaidi ya tembo wa kawaida. Tembo huishi miaka 60 hadi 70.

## Muundo wa kijamii na tabia


Makundi ya tembo huongozwa na jike mkubwa kuliko wote. Majike huishi katika makundi ambapo huwa hawachangamani na madume.

Makundi hujumuisha tembo 8 hadi 100 kulingana na eneo la ardhi na ukubwa wa familia.


Tembo dume wanaishi pekee yao na wakati mwingine huwa na makundi madogo ya muda. Madume huondoka katika familia wakiwa na umri wa miaka 10 mpaka 14.

Madume wanaofukuzwa kwenye kundi lao huunda makundi ya madume, lakini kuna ukorofi mkubwa kati yao kwa ajili ya kupigania nani atakayetawala kikundi hicho. Mvutano huu husababisha madume wengi kuchagua kuondoka kwenye kundi la Tembo dume na kuwa wenyewe.Ikiwa dume ni dhaifu sana anaweza kulazimika kutoka kwenye kundi hilo. Madume huumizana mara chache kimwili wakati wanapigania haki ya kuwa na jike. Mara nyingi dume wadogo hukaa mbali na wakubwa.

Tembo dume hutofautiana kimaumbile na tembo jike. Madume huwa na miili mikubwa iliyojengeka, vipaji vyao vya uso huwa vya mviringo. Majike huwa na vipaji vilivyochochongoka.



Tembo jike



Tembo dume










## Maelekezo ya Uzio wa Pilipili

### Hatua za kutengeneza.

- Chimba mashimo ya nguzo yenye umbali mita 7-10 kwa kila nguzo.
- Twanga pilipili kuwa chembe chembe nzuri, changanya na oil chafu (8 -10kg ya Pilipili kwa lita 10 za oil chafu).
- Kata vipande vya vitamba 15x10 sm (sentimita) na kufunga kila kona zake katika kamba ya katani.
- Loweka vitamba venye kamba za katani katika mchanganyiko wa mafuta yenye pilipili (oil chafu)
- Funga kamba za katani kwenye nguzo kwa kukaza, ukiacha njia moja tu kama mlango
- Angalau vipande vitatu vya vitambaa vya kotoni ziwe kati ya kila nguzo. Zungusha katika mipaka yote ya shamba.





### Uzio wa pilipili

Uzio wa pilipili unahitaji nyenzo ndogo ndogo na matengenezo, kwa vile unatumiwa wakati wa msimu wa mavuno, tofauti na uzio wa aina nyingine ambao unapaswa kukaa hadi mwaka. Uzio unatengenezwa na *kamba ya katani*, *nguzo*, *vitambaa*, *oil chafu*, *unga wa pilipili*, na zana mbalimbali za ujenzi wa uzio. Ili uzio uwe vizuri, ujenzi sahihi na matengenezo katika wakati sahihi wa mwaka ni muhimu. Ni bora kujenga uzio wakati mazao yamekaribia kukomaa na kukaribia mavuno (wiki 4-6 kabla ya mavuno).







# Njia za kuzuia Tembo kuingia mashambani

The Rufford Foundation www.rufford.org @ruffordgrants

LCMO Landscape and Conservation Mentors Organization


Baadhi ya picha kwa hisani ya Honeyguide Foundation na STE

Chapisho hili limefadhiliwa na Mradi wa Rufford

## Njia zingine




**Utumiaji wa honi zenye kelele**




**Matumizi ya tochi yenye mwanga mkali**



**Kuchoma Mchanganyiko wa kinyesi cha mifugo na pilipili**



**Fensi ya taa kuizunguka nyumba au ghala la mazao**



**Fensi ya umeme**

Tembo huitaji maeneo makubwa yaliyo na rasilimali za kutosha za chakula na maji. Kutokana na ukuaji wa idadi ya watu na uhitaji mkubwa wa rasilimali za asili, maeneo haya yamekua hatarini kuharibika na kupotea. Matokeo yake ni kuongezeka kwa mgongano baina ya wanadamu na tembo. Mgongano huu umepelekea majeraha na wakati mwingine kifo kwa binadamu, kupoteza mazao na uharibifu wa miundombinu. Hii pia imesababisha tembo kuuawa kama kulipiza kisasi. Wakati mwingine tembo wanaosababisha uharibifu huuawa na mamlaka husika.

## *Je wajua nyuki huzuia tembo kuvamia mashamba?*

Mgogoro baina ya binadamu na tembo umepelekea watafiti mbalimbali duniani kutafuta suluhisho la kudumu lisilo na madhara kwa viumbe hawa wawili. Moja katika ya njia hizi ni uzio wa mizinga ya nyuki. Mbinu hii ilivumbuliwa na mtafiti Lucy King ambae akiwa katika shughuli zake kawaida porini, aligundua kuwa tembo wanakwepa migunga yenye nyuki. Hii ilimpelekea kujaribisha kutumia mizinga ya nyuki kuzunguka mashamba.

Matokeo yake ni kuwa baada ya mizinga hio kuingiwa na nyuki, tembo walianza kukwepa mashamba yenye fensi ya mizinga. Mbinu hii imekuwa na mafanikio makubwa makubwa sana katika sehemu mbalimbali za bara Afrika na Asia. Majaribio ya fensi hizi Mang'ula Tanzania umeonyesha kuwa uwezekano wa tembo kuingia mashambani umepungua kwa asilimia 50 ikilinganishwa na kipindi cha nyuma kabla ya fensi kuwekwa.

Unachohitaji ni mizinga ya nyuki, nguzo za kushikilia mizinga na nyaya za kuunganisha mzinga kwa mzinga.


Fensi hii kuzunguka mashamba. Mbinu hii hufanya kazi vizuri uwepo wa nyuki ukiwa mkubwa. Hutoa faida ya asali huku ikisaidia uhifadhi wa tembo.




## Mifano ya fensi za mizinga ya nyuki












Landscape and Conservation Mentors Organization

**P.o. BOX 285, Mpanda Katavi**

**www.lcmo.or.tz**

Barua pepe: ***conservation@lcmo.or.tz***